Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Kwanza

## Ufunuo Wa Yesu Kristo

### Ufunuo Wa Yesu Kristo (Ufunuo 1:1-20)

*Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana;*

*Aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona.*

*Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.*

*Yohana, kwa yale makanisa saba yaliyoko Asia; Neema na iwe kwenu na amani, zitokazo kwake yeye aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja; na zitokazo kwa roho saba walioko mbele ya kiti chake cha enzi;*

*Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, shahidi aliye mwaminifu, mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mkuu wa wafalme wa dunia. Yeye atupendaye na kutuosha dhambi zetu katika damu yake,*

*Na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina.*

*Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.*

*Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.*

*Mimi Yohana, ndugu yenu na mwenye kushiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na subira ya Yesu Kristo, nalikuwa katika kisiwa kiitwacho Patmo, kwa ajili ya Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu.*

*Nalikuwa katika Roho, siku ya Bwana; nikasikia sauti kuu nyuma yangu, kama sauti ya baragumu,*

*Ikisema, Haya uyaonayo uyaandike katika chuo, ukayapeleke kwa hayo makanisa saba: Efeso, na Smirna, na Pergamo, na Thiatira, na Sardi, na Filadelfia, na Laodikia.*

*Nikageuka niione ile sauti iliyosema nami. Na nilipogeuka, niliona vinara vya taa saba vya dhahabu;*

*Na katikati ya vile vinara nikaona mtu mfano wa Mwanadamu, amevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi wa dhahabu matitini.*

*Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe, kama theluji; na macho yake kama mwali wa moto;*

Na miguu yake kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti yake kama sauti ya maji mengi.*

*Naye alikuwa na nyota saba katika mkono wake wa kuume; na upanga mkali, wenye makali kuwili, ukitoka katika kinywa chake; na uso wake kama jua liking'aa kwa nguvu zake.*

*Nami nilipomwona, nalianguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono wake wa kuume juu yangu, akisema, Usiogope, Mimi ni wa kwanza na wa mwisho,*

*Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.*

*Basi, uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayokuwa baada ya hayo.*

*Siri ya zile nyota saba ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, na ya vile vinara saba vya dhahabu. Zile nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba; na vile vinara saba ni makanisa saba.*

### Utangulizi Wa Mlango Wa Kwanza

Ufunuo 1:1-3.

"Ufunuo wa Yesu Kristo, aliopewa na Mungu awaonyeshe watumwa wake mambo ambayo kwamba hayana budi kuwako upesi; naye akatuma kwa mkono wa malaika akamwonyesha mtumwa wake Yohana;

Aliyelishuhudia Neno la Mungu, na ushuhuda wa Yesu Kristo, yaani, mambo yote aliyoyaona.

Heri asomaye na wao wayasikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyoandikwa humo; kwa maana wakati u karibu.“

Mwandishi (si mwanzilishi) wa kitabu hiki ni mtauwa Yohana Mt.. Wanahistoria wanakubaliana ya kwamba yeye aliishi sehemu ya mwisho ya maisha yake huko Efeso, ingawa katika wakati wa kuandika kitabu hiki yeye alikuwa katika Kisiwa cha Patmo. Si hadithi ya maisha ya Yohana, bali ni Ufunuo wa Yesu Kristo katika nyakati za kanisa zijazo. Katika aya ya tatu unaitwa unabii na ndivyo ilivyo hasa.

Kitabu hiki kwa kawaida huitwa Ufunuo wa Yohana Mtakatifu, lakini hilo si sahihi. Ni Ufunuo wa Yesu Kristo aliopewa Yohana kwa ajili ya Wakristo wa nyakati zote. Ndicho kitabu pekee katika Biblia nzima ambacho kimeandikwa na Yesu Mwenyewe, kwa kumtokea mwandishi Yeye Mwenyewe.

Ndicho kitabu cha mwisho cha Biblia, hata hivyo kinasimulia mwanzo na mwisho wa nyakati za Injili.

Sasa neno la Kiyunani la ufunuo ni “apocalypse” ambalo maana yake ni “kufunuliwa”. Kufunuliwa huku kunaelezewa kikamilifu katika mfano wa mchonga sanamu akifunua kazi yake ya sanamu, akiianika kwa mtazamaji. Ni kufunua, kuonesha kile kilichokuwa kimefichwa hapo awali. Sasa kule kufunua si tu ufunuo wa Utu wa Kristo, bali ni UFUNUO WA KAZI ZAKE ZIJAZO KATIKA ZILE NYAKATI SABA ZIJAZO.

*Umuhimu wa ufunuo wa Roho kwa mwaminio wa kweli hauwezi kamwe kutiliwa mkazo sana.* Ufunuo unamaanisha mengi zaidi kwako labda kuliko unavyotambua. Sasa sizungumzi juu ya Kitabu hiki cha Ufunuo na wewe. Ninazungumza juu ya mafunuo YOTE. Ni muhimu sana kwa kanisa. Je! unakumbuka katika Mathayo 16 ambapo Yesu aliwauliza wanafunzi swali hili,

“Watu husema mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?

Nao wakasema, Wengine husema ya kwamba Wewe u Yohana Mbatizaji; wengine Eliya; na wengine, Yeremia, ama mmoja wa manabii.

Akawaambia, Lakini ninyi je, mwasema mimi kuwa ni nani?

Ndipo Simoni Petro akajibu akamwambia, “Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

Naye Yesu akajibu akamwambia, “Heri wewe, Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye mbinguni.

Nami nakuambia, ya kwamba wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa Langu; wala malango ya kuzimu hayatalishinda.

Wakatoliki wa Kirumi wanasema ya kwamba kanisa limejengwa juu ya Petro. Sasa hilo kwa kweli ni la kimwili. Mungu angewezaje kulijenga kanisa juu ya mtu asiye na msimamo hata akamkana Bwana Yesu na kulaani wakati akifanya jambo hilo? Mungu hawezi kulijenga kanisa Lake juu ya mtu yeyote aliyezaliwa katika dhambi. Wala haikuwa ni mwamba fulani uliokuwa umelala pale kana kwamba Mungu alikuwa ameitakasa ardhi ya mahali pale. Na si kama Waprotestanti wanavyosema, kwamba kanisa limejengwa juu ya Yesu. Ilikuwa ni UFUNUO. Lisome jinsi lilivyoandikwa: “Mwili na damu HAVIKUKUFUNULIA hili, BALI BABA YANGU NDIYE ALIYEKUFUNULIA, na JUU YA MWAMBA HUU (UFUNUO) NITALIJENGA KANISA LANGU:” Kanisa limejengwa juu ya Ufunuo, juu ya “Bwana Asema Hivi”.

Habili alijuaje la kufanya ili kumtolea Mungu dhabihu ifaayo? Kwa imani alipokea ufunuo wa ile damu. Kaini hakupata ufunuo kama huo (hata ingawa alikuwa na amri) kwa hiyo asingeweza kutoa dhabihu sahihi. Ilikuwa ni ufunuo kutoka kwa Mungu ulioleta tofauti na kumpa Habili uzima wa milele. Sasa unaweza kuchukua yale mchungaji asemayo, ama yale seminari inayofundisha, na ingawa huenda ikafundishwa kwako kwa ufasaha wa maneno, mpaka Mungu atakapokufunulia ya kwamba Yesu ni Kristo, na kwamba ni damu inayokutakasa, na kwamba Mungu ni Mwokozi wako, kamwe hutapata uzima wa milele. Ufunuo wa Kiroho ndio unaofanya jambo hilo.

Sasa nilisema ya kwamba Kitabu hiki cha Ufunuo ni ufunuo wa Yesu na yale anayofanya makanisani kwa zile nyakati saba. Ni ufunuo kwa sababu wanafunzi, wao wenyewe, hawakujua kweli hizi zilizorekodiwa. Haikuwa imefunuliwa hapo awali kwao. Mnakumbuka ya kwamba walimjia Yesu katika Kitabu cha Matendo na kumwuliza, “Je! wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme?” Naye akasema, “Si kazi yako kujua nyakati wala majira.” Watu hao walikuwa wangali wakifikiria juu ya Yesu kuwa na ufalme wa duniani. Lakini ulikuwa ni ufalme wa kiroho ambao alikuwa anaenda kuujenga. Hata Yeye hakuweza kuwaambia kuhusu mahali Pake katika huo, kwa maana Baba hakuwa amemfunulia. Lakini sasa baada ya kifo Chake na kufufuka Kwake, na wakati huu hasa katika huduma Yake ya upatanisho, Yeye anaweza kuweka hapa katika ufunuo huu Wake Mwenyewe kwa Yohana kile utukufu Wake na uwepo wake kanisani ungemaanisha na kufanya.

Katika ufunuo huu anatuambia mwisho wa ibilisi ni nini. Yeye anasimulia jinsi atakavyomshughulikia

Ibilisi na kumtupa katika ziwa la moto. Yeye hufunua mwisho wa waovu wanaomfuata Shetani. Na Shetani huchukia jambo hilo.

Je! Umewahi kuona jinsi Shetani anavyochukia vitabu viwili vya Biblia kuliko vingine vyote? Kupitia wanatheolojia wenye mawazo huru na wanasayansi bandia yeye daima anashambulia Kitabu cha Mwanzo na Kitabu cha Ufunuo. Katika vitabu hivi viwili tunaona chimbuko la Shetani, njia zake mbaya sana na maangamizi yake. Hiyo ndiyo sababu anavishambulia. Yeye anachukia kufunuliwa, na katika vitabu hivyo anafunuliwa kwa kile hasa alicho. Yesu alisema kuhusu Shetani, "Yeye hana sehemu ndani Yangu wala sina sehemu ndani yake." Ibilisi angetaka kuthibitisha jambo hilo tofauti; bali yeye hawezi, kwa hiyo anafanya yote awezayo kuharibu imani katika Neno. Lakini wakati kanisa litakapokataa kumwamini Shetani na liamini ufunuo wa Roho wa Neno, milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.

Hebu niweke tu neno ndani hapa kutoka kwenye huduma yangu mwenyewe, kama hamjali. Nyote mnajua ya kwamba karama hii maishani mwangu ni ya kimbinguni. Ni karama ambayo kwayo Roho Mtakatifu anaweza kuyatambua magonjwa, na mawazo ya mioyo ya watu, na mambo mengine yaliyofichwa ambayo ni Mungu pekee angeweza kujua na kisha kunifunulia. Laiti mngeweza kusimama pamoja nami na kuona nyuso za watu wakati Shetani anapojua atafichuliwa. Sasa, si watu ninaozungumzia. Ni kwamba Shetani ameyashikilia katika maisha yao kwa dhambi, kutokujali, na maradhi. Lakini unapaswa kuona nyuso zao. Shetani anajua atafichuliwa, na mabadiliko ya kipekee sana huja juu ya nyuso za watu. Shetani anaogopa. Yeye anajua ya kwamba Roho wa Mungu yu karibu kuwajulisha watu kuhusu matendo yake. Hiyo ndiyo sababu anachukia mikutano hii sana. Wakati majina yanapoitwa na magonjwa yakifunuliwa, Shetani huchukia hilo. Sasa hii ni nini? Si kusoma mawazo, si kuwasiliana mawazo, wala si uchawi. Ni UFUNUO kwa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo njia pekee ninayoweza kujua jamba hilo. Bila shaka nia ya mtu wa kimwili italiita cho chote kile isipokuwa Roho Mtakatifu.

Hebu niwaonyeshe sababu nyingine kwa nini Shetani huchukia Kitabu hiki cha Ufunuo wa Yesu Kristo kanisani. Yeye anajua ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, na leo, na hata milele, Naye habadiliki. Yeye anajua hilo zaidi sana kuliko asilimia tisini ya wanatheolojia. Yeye anajua ya kwamba kwa kuwa Mungu habadiliki katika tabia Yake, basi Yeye pia habadiliki katika njia Zake. Hivyo basi Shetani anajua kwa hakika ya kwamba lile kanisa la asili pale Pentekoste lenye nguvu za Mungu (Marko kumi na Sita katika matendo) ndilo Kanisa Halisi ambalo Yesu anadai kama Lake. Mambo mengine yote ni ya uongo. Haina budi kuwa hivyo.

Sasa kumbukeni jambo hili. Kristo katika Kanisa la Kweli ni mwendelezo wa KITABU CHA MATENDO. Lakini Kitabu cha Ufunuo kinaonyesha jinsi ambavyo roho wa mpinga-Kristo angeingia kanisani na kulichafua, akilifanya kuwa vuguvugu, la kawaida na lisilo na nguvu. Inamfunua Shetani, ikifunua kazi zake (kujaribu kuangamiza watu wa Mungu na kupuuza neno la Mungu) moja kwa moja hadi wakati atakapotupwa katika ziwa la moto. Yeye anapinga jambo hilo. Hawezi kustahimili jambo hilo. Anajua ya kwamba kama watu wakipata UFUNUO WA KWELI wa KANISA LA KWELI na kile lilicho, msimamo wake ni nini na ya kwamba LINAWEZA KUTENDA ZILE KAZI KUBWA ZAIDI, hilo litakuwa jeshi lisiloweza kushindwa. Kama wakipata ufunuo wa kweli wa hizo roho mbili katika mfumo wa kanisa la Kikristo, na kwa Roho wa Mungu kutambua na kuhimili roho ya mpinga-Kristo, Shetani atakuwa hana nguvu mbele yake. Yeye atashindwa kabisa leo kama wakati Kristo alipopinga kila jitihada zake za kupata nguvu juu Yake jangwani. Naam, Shetani huchukia ufunuo. Lakini sisi tunaupenda huo. Tukiwa na ufunuo wa kweli maishani mwetu, malango ya kuzimu hayawezi kutushinda, bali tutayashinda.

Mtakumbuka ya kwamba nilitaja mwanzoni mwa ujumbe huu kwamba Kitabu hiki tunachojifunza ni ufunuo halisi wa Yesu, Mwenyewe, kanisani na kazi Yake katika nyakati zijazo. Ndipo nikataja ya kwamba inahitaji Roho Mtakatifu kutupa ufunuo la sivyo tutashindwa kuupata. Tukiyaleta pamoja mawazo haya mawili mtaona ya kwamba haitachukua tu kusoma kwa kawaida na kuwaza kukifanya Kitabu hiki kuwa halisi. Itachukua utendaji wa Roho Mtakatifu. Hiyo inamaanisha Kitabu hiki hakiwezi kufunuliwa kwa mtu yeyote ila tabaka maalum la watu. Itahitaji mtu aliye na ono la kinabii. Itahitaji uwezo wa kusikia kutoka kwa Mungu. Itahitaji mafundisho ya kimbinguni, si tu kwa mwanafunzi kulinganisha aya na aya,ingawa jambo hilo ni zuri. Lakini siri inahitaji mafundisho ya Roho ama sivyo halitakuwa dhahiri hata kidogo. Jinsi tunavyohitaji kusikia kutoka kwa Mungu na kujiweka wazi na kujisalimisha kwa Roho kusikia na kujua.

Kama nilivyokwisha sema, Kitabu hiki (Ufunuo) ni ukamilifu wa Maandiko. Hata kimewekwa sawa kabisa katika orodha ya Maandiko; mwishoni. Sasa unaweza kujua kwa nini hasa kinasema ya kwamba mtu ye yote anayekisoma ama hata kukisikia amebarikiwa. Ni ufunuo wa Mungu utakaokupa mamlaka juu ya ibilisi. Nawe unaweza kuona ni kwa nini wale ambao wangeongeza ama kuondoa kutoka kwake wangelaaniwa. Ingebidi kuwa hivyo, kwa maana ni nani anayeweza kuongeza ama kuondoa ufunuo mkamilifu wa Mungu na kumshinda adui? Ni rahisi hivyo. Hakuna kitu kilicho na nguvu za ushindi namna hiyo kama ufunuo wa Neno. Mnaona, katika aya ya tatu baraka inatangazwa kwa wale watakaokitegea sikio maalum Kitabu hiki. Nafikiri jambo hili linazungumzia desturi ya Agano la Kale kuhusu makuhani kuwasomea kusanyiko Neno asubuhi. Mnaona, wengi hawangeweza kusoma kwa hiyo ilibidi kasisi awasomee. Mradi tu lilikuwa ni Neno, baraka ilikuwapo. Haikujalisha kama ilisomwa au kusikilizwa.

"Wakati u karibu." Wakati haukuwa karibu hapo awali. Katika hekima na utaratibu wa Mungu ufunuo huu mkuu (ingawa ulijulikana kikamilifu na Mungu) usingeweza kuja kabla ya wakati huu. Kwa hiyo tunajifunza kanuni fulani mara moja—*ufunuo wa Mungu kwa ajili ya kila wakati unaweza kuja katika wakati huo peke yake, na katika wakati maalum.* Angalia historia ya Israeli. Ufunuo wa Mungu kwa Musa ulikuja tu katika wakati maalum wa historia, na hata zaidi hasa ulikuja wakati watu walipomlilia Mungu. Yesu, Mwenyewe, alikuja katika wakati mkamilifu, Yeye akiwa Ufunuo mkamilifu wa Uungu. Na katika wakati huu (Laodikia) ufunuo wa Mungu utakuja katika wakati wake. Hautakawia, wala hautakuwa kabla ya wakati wake. Liwazie hili na ulizingatie vizuri, kwa kuwa tuko katika wakati wa mwisho leo.

**Salamu**

Ufunuo 1:4-6.

"Yohana, kwa yale makanisa saba yaliyoko Asia; Neema na iwe kwenu, na amani, zitokazo Kwake Yeye Aliyeko, na Aliyekuwako, na Atakayekuja; na zitokazo kwa Roho saba walioko mbele ya kiti Chake cha enzi;

Tena zitokazo kwa Yesu Kristo, Shahidi aliye Mwaminifu, Mzaliwa wa Kwanza wa Waliokufa, na Mkuu wa Wafalme wa Dunia. Yeye atupendaye, na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake Mwenyewe,

Na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, na Baba Yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina."

Neno, Asia, kwa kweli ni Asia Ndogo. Ni kipande kidogo cha ardhi cha ukubwa kama wa Indiana kwa ukubwa. Hayo makanisa saba kule yalichaguliwa maalum miongoni mwa makanisa mengine yote kwa ajili ya tabia zao, tabia zile zile ambazo zingeonekana katika nyakati zilizofuata na karne nyingi baadaye.

Zile Roho saba mbele ya kile kiti cha enzi ni Roho aliyekuwa ndani ya kila mmoja wa wale wajumbe saba, akiwapa huduma zao kwa wakati ule ambao kila mmoja wao aliishi.

Sasa maneno yote haya, 'Yeye Aliyeko', na 'Aliyekuwako', na 'Atakayekuja', na 'Shahidi Mwaminifu', na 'Mzaliwa wa Kwanza wa Waliokufa', na 'Mkuu wa Wafalme wa Dunia', na 'Alfa na Omega', na 'Mwenyezi', ni sifa na maelezo ya MTU YULE YULE MMOJA, Ambaye ni Bwana Yesu Kristo, Ambaye alituosha dhambi zetu katika damu Yake Mwenyewe.

Roho wa Mungu ndani ya Yohana ananena namna hii kusudi aonyeshe Uungu Mkuu wa Yesu Kristo na kumfunua Mungu kama ni MUNGU MMOJA. Leo kuna kosa kubwa. Ni kwamba kuna Miungu watatu badala ya mmoja. Ufunuo huu kama alivyopewa Yohana na Yesu, Mwenyewe, husahihisha kosa hilo. Si kwamba kuna Miungu watatu, bali ni Mungu mmoja aliye na ofisi tatu. Kuna Mungu Mmoja mwenye vyeo vitatu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ufunuo huu mkuu ni ule uliokuwa na kanisa la mwanzoni, na hauna budi kurejeshwa katika siku hii ya mwisho pamoja na kanuni sahihi ya ubatizo wa maji.

Sasa wanatheolojia wa kisasa hawatakubaliana nami kwa kuwa hapa ndipo palipoandikwa katika gazeti kubwa la Kikristo. "Fundisho hilo (kuhusu Utatu) ndilo asili na kiini hasa cha Agano la Kale. Ni asili na kiini kabisa cha Agano Jipya. Agano Jipya linapinga tu kama Agano la Kale wazo kwamba kuna zaidi ya Mungu mmoja. Hata hivyo Agano Jipya kwa udhahiri ule ule linafundisha ya kwamba Baba ni Mungu, na Mwana ni Mungu, na Roho Mtakatifu ni Mungu, na ya kwamba hawa watatu SI sifa tatu za Mtu yule yule, bali ni watu watatu wakisimama kwa kweli katika uhusiano wa kibinafsi mmoja kwa mwingine. Hapo tuna lile fundisho kuu la Nafsi Tatu lakini ni Mungu mmoja."

Wanasema pia, "Mungu, kulingana na Biblia, si mtu mmoja tu, bali Yeye ni nafsi tatu katika Mungu mmoja. Hiyo ndiyo siri kuu ya Utatu".

Hakika ni kweli. Watu watatu wanawezaje kuwa katika Mungu mmoja? Si kwamba tu hakuna Biblia kwa ajili ya jambo hilo, lakini hata inaonyesha ukosefu wa kutumia akili. Watu watatu mbalimbali, ingawa wao wana maumbile sawa, wanafanya miungu watatu, la sivyo lugha imepoteza maana yake kabisa.

Hebu sikiliza maneno haya tena, "Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, asema Bwana, Aliyeko, na Aliyekuwako, na Atakayekuja, Mwenyezi". Huu ni Uungu. Huyu si nabii tu, mwanadamu. Huyu ni Mungu. Na si ufunuo wa Miungu watatu, bali wa MUNGU MMOJA, Mwenyezi.

Hawakuamini katika Miungu watatu mwanzoni mwa kanisa. Huwezi kupata imani ya namna hiyo miongoni mwa mitume. Ilikuwa ni baada ya wakati wa mitume ndipo nadharia hii ilipoingia na kweli ikawa hoja na fundisho kuu kwenye Baraza la Nikea. Fundisho la Uungu lilisababisha migawanyiko miwili hapo Nikea. Na kutokana na mgawanyiko huo kukatokea pande mbili zilizopita mpaka. Upande mmoja kweli uliingia katika imani ya miungu mingi, ukiamini katika Miungu watatu, na hao wengine wakaingia katika imani ya umoja. Bila shaka hilo lilichukua muda kutukia, bali lilitukia, na tunalo leo ii hii Lakini Ufunuo kupitia kwa Yohana kwa Roho kwa makanisa ulikuwa, "Mimi ni Bwana Yesu Kristo, nami ndimi YOTE hayo. Hakuna Mungu mwingine ye yote". Naye akaweka muhuri Wake juu ya Ufunuo huu.

Fikiria hili: Baba wa Yesu alikuwa nani? Mathayo 1:18 inasema, "Alionekana ana mimba kwa Roho Mtakatifu". Lakini Yesu, Mwenyewe, alidai ya kwamba Mungu alikuwa ni Baba Yake. Mungu Baba na Mungu Roho Mtakatifu, kama tunavyotumia maneno haya mara nyingi, yanamfanya Baba na Roho kuwa MMOJA. Kweli ndivyo walivyo, la sivyo Yesu alikuwa na Baba wawili. Lakini angalia kwamba Yesu alisema ya kwamba Yeye na Baba Yake walikuwa Mmoja—sio wawili. Hilo linamfanya Mungu MMOJA.

Kwa kuwa jambo hili ni kweli kihistoria na Kimaandiko, watu wanashangaa hao watatu walitoka wapi. Likawa fundisho la msingi katika Baraza la Nikea mnamo 325 A.D. Utatu huu (neno lisilo la kimaandiko kabisa) ulitokana na miungu mingi ya Rumi. Warumi walikuwa na miungu wengi ambayo waliitolea maombi. Pia waliomba kwa mababu kama wapatanishi. Ilikuwa ni hatua tu ya kuipa miungu ya kale majina mapya, kwa hiyo tuna watakatifu ili kulifanya la Kibiblia zaidi. Kwa hivyo, badala ya Jupiter, Venice, Mars, na kadhalika, tuna Paulo, Petro, Fatima, Christopher, na kadhalika. Hawakuweza kuifanya dini yao ya kipagani kufanya kazi na Mungu mmoja tu, kwa hiyo walimgawa sehemu tatu, nao wakawafanya watakatifu kuwa wapatanishi kama walivyokuwa wamefanya na mizimu yao.

Tangu wakati huo watu wameshindwa kutambua ya kwamba kuna Mungu mmoja tu aliye na ofisi tatu au madhihirisho. Wanajua kuna Mungu mmoja kulingana na Maandiko, bali wao wanajaribu kulifanya kuwa nadharia ya mazingaombwe kwamba Mungu ni kama kichala cha zabibu; nafsi tatu zote zikishiriki Uungu ule ule sawasawa. Lakini inasema dhahiri hapa katika Ufunuo ya kwamba Yesu ni "Yeye Aliyeko", "Yeye Aliyekuweko", na "Yeye Atakayekuja". Yeye ni "Alfa na Omega", ambalo linamaanisha ya kwamba Yeye ni "A mpaka Z" au HAYO YOTE. Yeye ni kila kitu—Mwenyezi. Yeye ni Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Bondeni, Nyota Yenye Kung'aa ya Asubuhi, Chipukizi la Haki, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Yeye ni Mungu, Mwenyezi Mungu. MUNGU MMOJA.

I Tim. 3:16 inasema, "Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu: Mungu alidhihirishwa katika mwili, akajulikana kuwa na haki katika Roho, akaonekana na malaika, akahubiriwa katika Mataifa, akaaminiwa katika ulimwengu, akachukuliwa juu katika Utukufu". Hivi ndivyo Biblia inavyosema. Haisemi kitu juu ya nafsi ya kwanza ama ya pili ama ya tatu hapa. Inasema Mungu alidhihirishwa katika mwili. Mungu Mmoja. Huyo MUNGU Mmoja alidhihirishwa katika mwili. Hilo linapaswa kutosheleza. Mungu alikuja katika umbo la mwanadamu. Hilo halikumfanya Yeye kuwa MUNGU MWINGINE. Yeye alikuwa MUNGU, MUNGU YEYE YULE. Ulikuwa ni ufunuo wakati huo, na ni ufunuo sasa. Mungu Mmoja.

Hebu na turudi nyuma katika Biblia na tuone kile alichokuwa hapo mwanzo kulingana na ufunuo aliotoa juu Yake Mwenyewe. Yehova mkuu alimtokea Israeli katika nguzo ya moto. Kama Malaika wa Agano Yeye aliishi katika ile nguzo ya moto na kuwaongoza Israeli kila siku. Hekaluni Yeye alitangaza kuja Kwake kwa wingu kuu. Ndipo siku moja Yeye alidhihirishwa katika mwili uliozaliwa na bikira uliokuwa umeandaliwa kwa ajili Yake. Mungu yule aliyefanya maskani Yake juu ya hema za Israeli sasa alijitwalia Mwenyewe hema ya mwili na akafanya maskani Yake kama mwanadamu kati ya wanadamu. Lakini Yeye alikuwa MUNGU YEYE YULE.

Biblia inafundisha ya kwamba MUNGU ALIKUWA NDANI YA KRISTO. MWILI huo ulikuwa ni Yesu. Katika Yeye ulikaa utimilifu wote wa Uungu, KWA JINSI YA MWILI. Hakuna kitu kinachoweza kuwa dhahiri zaidi ya hicho. Siri, ndiyo. Lakini ukweli halisi—hauwezi kuwa dhahiri. Kwa hiyo kama Yeye hakuwa watu watatu wakati huo, Yeye hawezi kuwa watatu sasa. MUNGU Mmoja: Na Mungu huyu huyu alifanyika mwili.

Yesu alisema, "Nilitoka kwa Mungu na ninaenda (kurudi) kwa Mungu". Yohana 16:27-28. Hilo ndilo hasa lililotukia. Yeye alitoweka duniani kwa njia ya mauti Yake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa. Ndipo Paulo akakutana Naye njiani akienda Dameski na akasema na Paulo na kusema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?" Paulo alisema, "U nani Wewe, Bwana?" Yeye alisema, "Mimi ni Yesu." Yeye alikuwa nguzo ya moto, nuru inayopofusha. Yeye alikuwa amerudi tena kuwa, sawasawa tu na vile alivyosema angekuwa. Akarudi katika namna ile ile aliyokuwa kabla hajachukua maskani ya mwili. Hivyo ndivyo hasa Yohana alivyoliona. Yohana 1:18 "Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mwana wa pekee, aliye katika kifua cha Baba, Yeye amemfunua". Angalia mahali Yohana anaposema ya kwamba Yesu YUKO. Yeye yuko NDANI ya kifua cha Baba.

Luka 2:11 inasema,

"Kwa maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa Mwokozi, ambaye ni Kristo Bwana".

Alizaliwa Kristo, na siku nane baadaye alipotahiriwa aliitwa Yesu, hata kama malaika alivyowaambia. Nilizaliwa Branham. Nilipozaliwa walinipa jina la William. Yeye alikuwa ni Kristo bali alipewa jina hapa chini miongoni mwa wanadamu. Hiyo maskani ya nje ambayo watu wangeweza kuona ilikuwa inaitwa Yesu. Yeye alikuwa Bwana wa Utukufu, Mwenyezi akidhihirishwa katika mwili. Yeye ni Mungu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Yeye ni yote hayo.

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni vyeo tu. Hayo si majina. Hiyo ndiyo sababu tunabatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo, kwa kuwa hilo ni jina, si cheo. Ni jina la vyeo hivyo, kama tu vile

unavyomchukua mtoto mchanga aliyezaliwa ambaye ni mwana na kumpa jina. Mtoto mchanga ndivyo alivyo, mwana ni cheo, ndipo unamtaja, John Henry Brown. Hubatizi tu katika 'Jina la Yesu'. Kuna maelfu ya akina Yesu duniani na hata walikuwako kabla ya Yesu, Mwokozi wetu. Lakini kuna mmoja tu aliyezaliwa Kristo, "Bwana Yesu Kristo".

Watu huzungumza juu ya Yesu kuwa Mwana wa Milele wa Mungu. Sasa hilo si ni kupingana? Ni nani aliyepata kusikia juu ya "Mwana" kuwa ni wa milele? Wana wana mianzo, lakini kile kilicho cha milele hakina mwanzo kamwe. Yeye ni Mungu wa Milele (Yehova) aliyedhihirishwa katika mwili.

Katika Injili ya Mtakatifu Yohana inasema,

"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

Alikuwa ni Shahidi wa Kweli na Mwaminifu kwa Neno la milele la Baba. Yeye alikuwa ni Nabii na angeweza kusema yale Baba aliyomwambia aseme. Yeye alisema, "Baba Yangu yu ndani Yangu". Hivyo ndivyo Yesu maskani alivyosema, "Baba Yangu yu ndani Yangu".

Mungu ana sifa nyingi: 'Haki yetu', na 'Amani yetu', na 'Aliyeko Daima', na 'Baba', na 'Mwana', na 'Roho Mtakatifu'; lakini ana jina moja tu la kibinadamu na jina hilo ni Yesu.

Usichanganyikiwe kwa sababu yeye ana afisi tatu ama kwamba Yeye ana dhihirisho mara tatu. Duniani Yeye alikuwa ni Nabii; mbinguni Yeye ni Kuhani; na kurudi duniani, Yeye ni Mfalme wa Wafalme. "Yeye Aliyekuwa" —Huyo ni Yesu, Nabii. "Aliyeko"—Huyo ni Yeye, Kuhani Mkuu, akifanya upatanisho—Yeye anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. "Atakayekuja" —Huyo ni yule Mfalme ajaye. Duniani Yeye alikuwa Neno—Nabii. Musa alisema kumhusu Yeye, "Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama mimi, na itakuwa kwamba wasipoyasikia maneno ya Nabii huyo watakatiliwa mbali na watu".

Angalia mambo haya kuhusu Yesu. Duniani Yeye alikuwa Nabii, Mwana-Kondoo, na Mwana. Hili halikumfanya kuwa watatu. Haya yalikuwa ni madhihirisho tu ama afisi za Mtu Mmoja, Yesu.

Sasa kuna sehemu inayopendwa sana ya Maandiko ambayo wa utatu wanafikiri huthibitisha hoja yao ya zaidi ya Nafsi moja halisi katika Uungu.

Ni Ufunuo 5:6-8,

"Nikaona, na, tazama, katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wanne, na katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

Akaja akakitwaa kile kitabu katika mkono wa kuume Wake Yeye aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi.

Hata alipokitwaa kile kitabu, hao wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne wakaanguka mbele za Mwana-Kondoo, kila mmoja wao ana kinubi, na vitasa vya dhahabu vilivyojaa manukato, ambayo ni maombi ya watakatifu."

Hakika aya hizi, zikitengwa, zingeonekana kuthibitisha wazo lao. Angalia, nilisema, aya hizi ZILIZOTENGWA.

Hata hivyo, soma Ufunuo 4:2-3 na 9-11,

"Na mara nalikuwa katika Roho: na tazama, kiti cha enzi kimewekwa mbinguni, na MMOJA ameketi juu ya kile kiti.

Na Yeye aliyeketi alionekana mithili ya jiwe la yaspi na akiki: na upinde wa mvua ulikizunguka kile kiti cha enzi, ukionekana mithili ya zumaridi.

Na hao wenye uhai wanapompa Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi utukufu na heshima na shukrani, Yeye aliye hai hata milele na milele,

Ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele Zake Yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, nao humsujudia Yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema,

Umestahili Wewe, Ee Bwana, kuupokea utukufu na heshima na uweza: kwa kuwa Wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi Yako vilikuwako, navyo vikaumbwa."

Angalia kwa makini katika kifungu cha pili inasema, "Mmoja" (si wawili ama watatu bali ni Mmoja) aliketi kwenye kiti cha enzi. Katika kifungu cha tatu inasema, "Yeye" (SI wao) alipaswa kuonekana kama jiwe la yaspi. Katika aya ya tisa inasema ya kwamba wale wanyama walimpa "YEYE" heshima (si wao).

Katika aya ya kumi inasema ya kwamba wale wazee walianguka mbele "ZAKE" (si yao). Katika aya ya kumi na moja inasema ya kwamba wakisema kwa sauti kuu, "Umestahili, EE BWANA" (si Mabwana). Na pia katika aya ya kumi na moja inasema huyu MMOJA kwenye kiti cha enzi alikuwa ndiye "Muumba", Ambaye ni Yesu (Yohana 1:3), Ambaye ni Yehova-Roho-Mungu wa Agano la Kale (Mwa. 1:1).

Lakini hebu tusikomee hapo. Soma sasa katika Ufunuo 3:21,

"Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti Changu cha enzi, kama vile vile mimi nilivyoshinda, na kuketi pamoja na Baba Yangu katika kiti Chake cha enzi."

Pia soma Waebrania 12:2,

"Tukimtazama Yesu Mwenye Kuanzisha na Mwenye Kutimiza imani yetu; Ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba, na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu."

Angalia ya kwamba kulingana na Yesu, Mwenyewe, Ambaye aliandika Ufunuo, Yeye ameketi PAMOJA na Baba. Roho ndani ya Paulo (Roho Ambaye ni Roho wa Kristo, kwa maana huyo ni Roho wa Unabii Ambaye huleta Neno) anasema Yeye ameketi MKONO WA KUUME wa Mungu. Lakini Yohana alipoangalia aliona "Mmoja" tu juu ya kiti cha enzi. Na haikuwa mpaka Ufunuo 5:6-8 (inayofuata Ufunuo 4:2-3 katika mfuatano wa wakati) ambapo ndipo tunamwona "Mwana-Kondoo" akitwaa kile kitabu kutoka kwa "Yeye" aliyeketi kwenye kiti cha enzi, kama inavyooneshwa katika Ufunuo 4 : 2-3 na 9-10. Ni kitu gani? Ni siri ya "MUNGU Mmoja." Yeye (Yesu), alitoka kwa Mungu, akadhihirishwa katika mwili, akafa na kufufuka tena, na akarudi kwenye "Kifua cha Baba." Kama alivyosema Yohana, "Mwana pekee Aliye NDANI ya kifua cha Baba, Huyu NDIYE aliyemfunua." Yohana 1:18. Ulikuwa sasa wakati wa Mungu (Masihi) kurudi kudai bibi-arusi Wake kisha ajitambulishe (ajitambulishe) kwa Israeli. Kwa hivyo tunamwona Mungu tena akija kuchukua uhusiano wa kimwili na mwanadamu kama "Mwana wa Daudi, Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, na Bwana Arusi wa Bibi-arusi Mmataifa." Sio Miungu "Wawili," bali ni MUNGU Mmoja tu akidhihirisha ofisi Zake kuu za utatu na vyeo.

Watu walijua Yeye alikuwa ni Nabii. Walijua ishara ya Masihi ambayo ingeweza kuja tu kupitia kwa nabii. Yohana 1:44-51,

"Naye Filipo alikuwa wa Bethsaida, mji wa Andrea na Petro.

Filipo akamwona Nathanaeli, akamwambia, Tumemwona yeye, ambaye Musa aliandika habari zake katika torati na manabii, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.

Nathanaeli akamwambia, Je! Laweza jambo jema kutoka Nazareti? Filipo akamwambia, Njoo uone.

Basi Yesu akamwona Nathanaeli anakuja Kwake, akanena habari zake, Tazama Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake!

Nathanaeli akamwambia, Umepataje kunitambua? Yesu akajibu, akamwambia, Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.

Nathanaeli akajibu, akamwambia, Rabi, Wewe u Mwana wa Mungu; Wewe ni Mfalme wa Israeli.

Yesu akajibu, akamwambia, Kwa sababu nilikuambia, Nilikuona chini ya mtini, waamini? utaona mambo makuu kuliko haya.

Naye akamwambia, Amin, amin, nawaambia, Tangu sasa mtaona mbingu zimefunguka, na malaika wa Mungu wakipaa na kushuka juu ya Mwana wa Adamu.

Uwezo wa kupambanua mawazo ya moyo katika wanadamu ulimfanya mteule wa Mungu kufahamu ya kwamba huyu hapa alikuwa Masihi, Neno lililotiwa mafuta la Mungu.

Waebrania 4:12,

"Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

Wakati yule mwanamke kisimani alipomsikia Yeye akiyatambua mawazo ya moyo wake huyo mwanamke alimkiri Yeye kama nabii, akitangaza ya kwamba Masihi atajulikana kwa uwezo huo mkuu.

Yohana 4:7- 26,

"Akaja mwanamke Msamaria kuteka maji: Yesu akamwambia, Nipe maji ninywe.

(Kwa maana wanafunzi wake walikuwa wameenda mjini kununua chakula).

Basi yule mwanamke Msamaria akamwambia, Imekuwaje Wewe, Myahudi, kutaka maji kwangu, nami ni mwanamke Msamaria? maana Wayahudi hawachangamani na Wasamaria.

Yesu akajibu akamwambia, Kama ungaliijua karama ya Mungu, naye ni Nani akuambiaye, Nipe maji ninywe, ungalimwomba Yeye, Naye angalikupa maji yaliyo hai.

Yule mwanamke akamwambia, Bwana, huna kitu cha kutekea, na kisima ni kirefu: basi umeyapata wapi hayo maji yaliyo hai?

Je! Wewe u mkubwa kuliko baba yetu Yakobo, aliyetupa kisima hiki, naye mwenyewe akanywa maji yake, na wanawe pia, na wanyama wake?

Yesu akajibu, akamwambia, Kila anywaye maji haya ataona kiu tena;

Walakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa Mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujikia uzima wa milele.

Yule mwanamke akamwambia, Bwana, unipe maji hayo, nisione kiu, wala nisije hapa kuteka.

Yesu akamwambia, Nenda kamwite mumeo, uje naye hapa.

Yule mwanamke akajibu, akasema, Sina mume.

Yesu akamwambia, Umesema vema, sina mume.

Kwa maana umekuwa na waume watano; na uliye naye sasa siye mume wako; katika hayo umesema kweli.

Yule mwanamke akamwambia, Bwana, naona ya kwamba Wewe u nabii.

Baba zetu waliabudu katika mlima huu; nanyi husema ya kwamba huko Yerusalemu ni mahali patupasapo kuabudia.

Yesu akamwambia, Mama, unisadiki, saa inakuja, ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala kule Yerusalemu.

Ninyi mnaabudu msichokijua: sisi tunaabudu tukijuacho: kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi.

Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli: kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu.

Mungu ni Roho; nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na katika kweli.

Yule mwanamke akamwambia, Najua ya kuwa yuaja Masihi, aitwaye Kristo: Naye atakapokuja, Yeye atatufunulia mambo yote.

Yesu akamwambia, Mimi ninayesema nawe, Ndiye.‶

Katika Ufunuo 15:3 inasema,

Katika Ufu. 15:3 inasema, "Nao wauimba wimbo wa Musa mtumwa wa Mungu, na wimbo wa MWANA-KONDOO, wakisema, Ni makuu na ya ajabu matendo Yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; ni za haki na za kweli njia Zako, Ee Mfalme wa Watakatifu."

Mnaona jambo hilo? Yule MWANAKONDOO, Kuhani Mkuu anayeshikilia damu Yake kama upatanisho kwenye kiti cha rehema kwa ajili ya dhambi zetu ni Bwana Mungu Mwenyezi. Hiyo ndiyo kazi Yake ya sasa. Hivyo ndivyo anavyofanya sasa, akiisihi damu Yake kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini siku moja Mwana-Kondoo huyo atakuwa Simba wa Kabila la Yuda. Yeye atakuja katika nguvu na utukufu na kuchukua mamlaka Yake kutawala kama Mfalme. Yeye ndiye Mfalme anayekuja wa dunia hii. Bila shaka, hilo halisemi Yeye si Mfalme sasa. Kwa kuwa Yeye ni Mfalme wetu, Mfalme wa Watakatifu. Sasa hivi ni ufalme wa kiroho. Si wa utaratibu wa ulimwengu huu kama vile sisi tusivyo wa ulimwengu huu. Hiyo ndiyo sababu tunatenda tofauti na ulimwengu. Uraia wetu uko mbinguni. Tunarudisha nuru ya Roho ya ulimwengu wa kuzaliwa kwetu upya ambapo Yesu ndiye Mfalme. Hiyo ndiyo sababu wanawake wetu hawavai mavazi ya wanaume ama kukata nywele zao ama kutumia vipodozi hivyo vyote na vitu vingine ambavyo ulimwengu unavipenda sana. Hiyo ndiyo sababu watu wetu hawakunywa pombe wala kuvuta sigara na kufanya dhambi. Utawala wetu ni utawala juu ya dhambi na unafanya kazi kwa nguvu zilizo katika Roho wa Kristo Anayeishi ndani yetu. Kila ufalme duniani utabomolewa, lakini wetu utabaki.

Sasa tumekuwa tukizungumza juu ya ofisi na madhihirisho ya Mungu mmoja wa kweli na kuuona utukufu Wake katika utafiti wa Kimaandiko. Lakini Yeye hapaswi kujulikana kiakili. Yeye anajulikana Kiroho; kwa ufunuo wa Kiroho. Mtu yuyu huyu aliyejulikana kama Yesu kwa jinsi ya mwili alirudi kwenye nguzo ya moto. Lakini Yeye aliahidi angerudi tena na kukaa kati ya watu Wake kwa Roho. Na kwenye siku

ya Pentekoste ile nguzo ya moto ilishuka na kujigawa yenyewe katika ndimi za moto juu ya kila mmoja wao. Mungu alikuwa akifanya nini? Alikuwa akijitenga Mwenyewe kanisani, akiwapa hao wanaume na wanawake sehemu Yake Mwenyewe. Alijigawanya Mwenyewe miongoni mwa kanisa Lake kama tu alivyosema angefanya.

Yohana 14:16-23,

"Nami nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine, apate kukaa nanyi milele;

Hata Roho wa Kweli: Ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni, wala haumjui Yeye; bali ninyi mnamjua; kwa maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.

Sitawaacha ninyi yatima; nitakuja kwenu.

Bado kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mnaniona: na kwa sababu Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.

Siku ile mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba Yangu, nanyi ndani Yangu, nami ndani yenu.

Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye: naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu, Nami nitampenda, na kujidhihirisha kwake.

Yuda akamwambia, si Iskariote, Bwana, imekuwaje kwamba ujidhihirishe kwetu, wala si kwa ulimwengu?

Yesu akajibu akamwambia, Mtu akinipenda, atayashika maneno Yangu: na Baba Yangu atampenda, Nasi tutakuja kwake, na kufanya makao Yetu kwake."

Yeye alisema ya kwamba angemwomba Baba Ambaye angemtuma Msaidizi mwingine Ambaye alikuwa PAMOJA nao (hao wanafunzi) tayari lakini SI NDANI yao. Huyo alikuwa ni Kristo. Halafu katika aya ya ishirini na tatu, akinena habari Zake Mwenyewe na za Baba, Yeye alisema NASI tutakuja. Hilo hapo: "Roho anakuja, Roho Yule Yule wa Mungu aliyejidhihirisha kama Baba, na kama Mwana, na angali atajidhihirisha katika wengi"—MUNGU MMOJA Ambaye ni Roho.

Hiyo ndiyo sababu hakuna mtu anayeweza kuja na kusema mtu mtakatifu ni papa au mtu mtakatifu ni askofu ama kasisi. MTU MTAKATIFU ni Kristo, Roho Mtakatifu, ndani yetu. Vipi viongozi wa dini watangaze kwamba washiriki hawana neno la kusema? Kila mmoja ana jambo la kusema. Kila mmoja ana kazi, kila mmoja ana huduma. Roho Mtakatifu alikuja katika Pentekoste na kujitenga Mwenyewe juu ya kila mmoja, kusudi litimizwe ambalo Kristo alisema,

"Siku ile mtajua ya kwamba Mimi niko ndani ya Baba Yangu, nanyi ndani Yangu na Mimi ndani yenu."

Yohana 14:20.

Yule Mimi Niko aliye Mkuu, Mwenyezi Mungu, amekuja kama Roho kulijaza kanisa Lake la kweli. Yeye ana haki ya kwenda mahali po pote anapotaka, na juu ya mtu ye yote anayetaka. Sisi hatufanyi "watu watakatifu" wo wote kati yetu, lakini kusanyiko lote la kweli la Mungu ni takatifu, kwa sababu ya uwepo wa Roho Mtakatifu. Yeye, Roho Mtakatifu, Ndiye aliye mtakatifu, si kusanyiko lenyewe lilivyo.

Sasa huo ndio ufunuo: Yesu Kristo ni Mungu. Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa lile Jipya. Haidhuru unajaribu vipi, huwezi kuthibitisha kuna Miungu WATATU. Lakini pia inahitaji ufunuo wa Roho Mtakatifu kukufanya ufahamu ukweli kwamba Yeye ni Mmoja. Inahitaji ufunuo kuona ya kwamba Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa lile Jipya. Shetani aliingia ndani ya kanisa na kuwapofusha watu wasione kweli hii. Na wakati walipopofushwa kwa jambo hilo, haikuchukua muda mrefu mpaka Kanisa la Rumi lilipoacha kubatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

Ninakiri ya kwamba inatakiwa ufunuo wa kweli kutoka kwa Roho Mtakatifu kuona ukweli juu ya Uungu siku hizi wakati tuko katikati ya kupotoshwa kwa Maandiko mengi sana. Lakini kanisa lenye nguvu, lenye kushinda limejengwa juu ya ufunuo kwa hiyo tunaweza kumtarajia Mungu kufunua kweli Yake kwetu. Hata hivyo, kwa kweli huhitaji ufunuo juu ya ubatizo wa maji. Uko papo hapo ukikukodolea macho usoni. Je! ingewezekana katika muda mfupi sana kwa mitume kuongozwa vibaya kutoka kwenye amri ya moja kwa moja ya Bwana kubatiza katika Jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu na halafu uwakute katika kutotii makusudi? Wao walijua hilo Jina lilikuwa ni lipi, na hakuna hata mahali pamoja katika Maandiko ambapo wao walibatiza katika njia nyingine yo yote nje ya Jina la Bwana Yesu Kristo. Akili ya kawaida ingekwambia ya kwamba Kitabu cha Matendo ni kanisa katika matendo, na kama wao walibatiza namna hiyo, basi hivyo ndivyo inavyopasa kubatiza. Sasa kama unafikiri hilo lina nguvu, unafikiri nini juu ya jambo hili? Mtu ye yote ambaye hakubatizwa katika Jina la Bwana Yesu ilibidi abatizwe tena.

Matendo 19:1-6: "Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo akiisha kupita kati ya nchi za juu, akafika Efeso: akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko, akawauliza, Je! Mlipokea Roho Mtakatifu tangu

mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia. Akawaambia, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema, Kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akasema, Yohana kweli alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini Yeye atayekuja nyuma yake, yaani, Kristo Yesu. Waliposikia jambo hili, walibatizwa katika Jina la Bwana Yesu. Na Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akawashukia; nao wakanena kwa lugha na kutabiri." Hivyo ndivyo ilivyo. Hawa watu wazuri huko Efeso walikuwa wamesikia juu ya Masihi ajaye. Yohana alikuwa amemhubiri. Wao walikuwa wamebatizwa wapate ondoleo la dhambi zao, wakitazamia MBELE wapate kuja kumwamini Yesu. Lakini sasa ilikuwa ni wakati wa kuangalia NYUMA kwa Yesu na kubatizwa ili kupata ONDOLEO la dhambi. Ulikuwa ni wakati wa kumpokea Roho Mtakatifu. Na walipobatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Paulo aliweka mikono yake juu yao na Roho Mtakatifu akaja juu yao.

Loo! hao watu wapendwa huko Efeso walikuwa ni watu wazuri; na kama mtu ye yote alikuwa na haki ya kujisikia salama, wao walijisikia. Angalia umbali waliokuwa wamekuja. Walikuwa wamesafiri wakafikia umbali wa kumkubali Masihi ajaye. Walikuwa tayari kwa ajili Yake. Lakini huoni ya kwamba ingawa walifanya hivyo walikuwa wamemkosa? Alikuwa amekuja na kuondoka. Walihitaji kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Walihitaji kujazwa na Roho Mtakatifu.

Kama umebatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, Mungu atakujaza na Roho Wake. Hilo ni Neno.

Matendo 19:6 ambayo tunasoma ilikuwa kutimizwa kwa Matendo 2:38,

"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."

Mnaona, Paulo, kwa Roho Mtakatifu, alisema yale hasa Petro aliyosema kwa Roho Mtakatifu. Na lililosemwa HALIWEZI kubadilishwa. Halina budi kuwa vile vile tangu Pentekoste mpaka yule wa mwisho kabisa aliyeteuliwa amebatizwa.

Wagalatia 1:8,

"Lakini ijapokuwa sisi, au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe."

Sasa baadhi yenu ninyi watu wa Umoja mnabatiza makosa. Mnabatiza kwa ajili ya kuzaliwa upya kama kwamba kuzamishwa majini huwaokoa. Kuzaliwa upya hakuji kwa njia ya maji; ni kazi ya Roho. Yule mtu ambaye kwa Roho Mtakatifu alitoa ile amri, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina la Bwana Yesu," hakusema ya kwamba maji yalileta kuzaliwa upya. Yeye alisema ilikuwa tu ni ushuhuda wa "dhamiri safi mbele za Mungu." Ilikuwa ni hayo tu.

I Petro 3:21,

"Mfano wa mambo hayo ni ubatizo unaotuokoa sisi pia siku hizi (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu,) kwa kufufuka Kwake Yesu Kristo."

Ninaamini jambo hilo.

Kama mtu ye yote analo wazo lo lote la uongo ya kwamba historia inaweza kuthibitisha ubatizo wa maji katika njia nyingine yo yote mbali na Jina la Bwana Yesu Kristo, ningekushauri usome historia na ujionee mwenyewe. Ifuatayo ni kumbukumbu ya kweli ya Ubatizo uliofanyika huko Rumi 100 B.K. na ukatolewa tena katika Gazeti la TIME la tarehe 5 Disemba, 1955. "Yule Shemasi akainua mkono wake, naye Publius Decius akaingia kwenye mlango wa mahali pa kubatizia. Marcus Vasca muuza kuni alikuwa amesimama katika kile kidimbwi maji yamemfikia kiunoni. Alikuwa anatabasamu wakati Publius alipokuwa akipita katika kidimbwi akaja akasimama karibu naye. 'Credis?' akauliza. 'Credo,' akajibu Publius. 'Ninaamini ya kwamba wokovu wangu unatoka kwa Yesu aliye Kristo, Ambaye alisulubishwa chini ya Pontio Pilato. Pamoja Naye nilikufa ili kwamba pamoja Naye nipate Uzima wa Milele. Ndipo akasikia mikono yenye nguvu ikimshikilia huku yeye akijiachilia kuanguka kinyumenyume katika kile kidimbwi, ndipo akasikia sauti ya Marcus kwenye sikio lake_ 'Nakubatiza katika Jina la Bwana Yesu'_huku maji baridi yakimfunika."

Hadi mpaka ile kweli ilipopotea (na haikurudi mpaka wakati huu wa mwisho_hii ni kutoka Nikea mpaka mwisho wa karne hii) walibatiza katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Lakini umerudi. Shetani hawezi kuuzuia ufunuo wakati Roho anataka kuutoa.

Naam, kama kungalikuweko na Miungu watatu, ungaliweza kubatiza kweli kwa Baba fulani, na Mwana fulani, na Roho Mtakatifu fulani. Lakini ule UFUNUO ALIOPEWA YOHANA ulikuwa kwamba KUNA MUNGU MMOJA na Jina Lake ni BWANA YESU KRISTO, nawe unabatiza kwa Mungu MMOJA na mmoja tu. Hiyo ndiyo sababu Petro alibatiza jinsi alivyobatiza katika Pentekoste. Ilimbidi awe mwaminifu kwa ufunuo ambao ulikuwa, "Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini, ya kwamba Mungu amemfanya YESU HUYO, mliyemsulibisha, kuwa BWANA NA KRISTO PIA." Huyo hapo, "BWANA YESU KRISTO."

Kama Yesu ni Bwana na Kristo 'PIA,' basi Yeye (Yesu) ni, na hawezi kuwa mwingine ila "Baba, Mwana,

na Roho Mtakatifu" katika Nafsi MOJA aliyedhihirishwa katika mwili. SI "Mungu katika nafsi tatu, utatu uliobarikiwa," bali ni MUNGU MMOJA, NAFSI MOJA yenye sifa tatu kuu, yenye afisi tatu zinazodhihirisha sifa hizo. Lisikieni mara nyingine tena. Yesu huyu huyu ni Bwana na Kristo "PIA." Bwana (Baba) na Kristo (Roho Mtakatifu) ni Yesu, kwa sababu Yeye (Yesu) ni wote WAWILI (Bwana na Kristo).

Kama hilo halituonyeshi ufunuo wa kweli wa Uungu, hakuna kitakachotuonyesha. Bwana SI mwingine; Kristo SI mwingine. Huyu Yesu ni Bwana Yesu Kristo—MUNGU Mmoja.

Filipo siku moja alimwambia Yesu, "Bwana, utuonyeshe Baba na itatutosha." Yesu akamwambia, "Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote wewe usinijue? Aliyeniona Mimi amemwona Baba, basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba? Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Nilinukuu hilo wakati mmoja na bibi mmoja akasema, "Hebu kidogo, Bw. Branham, wewe na mke wako ni mmoja."

Nikasema, "Si kwa namna hiyo."

Akasema, "Samahani?"

Kwa hiyo nikamwambia, "Unaniona?"

Akasema, "Naam."

Nikasema, "Unamwona mke wangu?"

Akasema, "La."

Nikasema, "Basi umoja huo ni wa aina tofauti, kwa kuwa Yeye alisema, Ukiniona Mimi, unamwona Baba."

Nabii alisema ya kwamba ingekuwako nuru wakati wa jioni. Katika wimbo imeandikwa:

"Kutakuwako nuru wakati wa jioni,
Njia ya kwenda utukufuni hakika mtaiona,
Katika njia ya maji, hiyo ndiyo nuru leo,
Ukizikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia ndani.
Nuru ya jioni imekuja—
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni mmoja.

Si muda mrefu sana uliopita nilikuwa ninazungumza na Rabi Myahudi. Akaniambia, "Ninyi Mataifa hamwezi kumkata Mungu vipande vitatu na kumpa Myahudi. Tunajua vizuri zaidi kuliko hivyo."

Nikamwambia, "Hivyo ndivyo ilivyo hasa Rabi, hatumkati Mungu katika vipande vitatu. Mnaamini manabii, sivyo?"

Akasema, "Hakika ninaamini."

"Mnaamini Isaya 9:6?"

"Naam."

"Nabii alikuwa akinena habari za nani?"

"Masihi."

Nikasema, "Masihi atakuwa na uhusiano gani na Mungu?"

Yeye alisema, "Yeye atakuwa Mungu."

Nikasema, "Hiyo ni kweli." Amina.

Huwezi kumweka Mungu katika nafsi tatu ama sehemu tatu. Huwezi kumwambia Myahudi ya kwamba kuna Baba fulani, na Mwana fulani, na Roho Mtakatifu fulani. Yeye atakwambia upesi sana ambapo wazo hilo lilitoka. Wayahudi wanajua kanuni hii ya imani ilianzishwa kwenye Baraza la Nikea. Si ajabu wao wanatudhihaki kama makafiri.

Tunazungumza juu ya Mungu asiyebadilika. Wayahudi wanaamini jambo hilo pia. Lakini kanisa lilimbadilisha Mungu wake asiyebadilika kutoka MMOJA kuwa WATATU. Lakini ile nuru inarudi wakati wa jioni. *Ni ajabu iliyoje ya kwamba ukweli huu umekuja katika wakati ambapo Wayahudi wanarudi Palestina.* Mungu na Kristo ni MMOJA. Yesu huyu ni BWANA NA KRISTO PIA.

Yohana alikuwa na ufunuo, na YESU ndiye aliyekuwa Ufunuo huo, Naye amejionyesha Mwenyewe papa hapa katika Maandiko_MIMI Ndiye Aliyekuwako, Aliyeko na Atakayekuja, Mwenyezi. Amina."

Kama ufunuo umekupita, angalia juu na umtafute Mungu uupate. Hivyo ndivyo tu utakavyoupata. Ufunuo hauna budi kuja kutoka kwa Mungu. Hauji kamwe kwa majaliwa ya kibinadamu, ya kawaida, bali kwa uvumilivu wa Kiroho. Unaweza hata kukariri Maandiko, na ingawa hilo ni zuri sana, hilo halitafaa kitu. Haina budi kuwa ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Inanenwa katika Neno ya kwamba hakuna mtu anayeweza kusema ya kwamba Yesu ndiye Kristo ila kwa Roho Mtakatifu. Huna budi kumpokea Roho Mtakatifu na ndipo, na ndipo tu, Roho anapoweza kukupa ufunuo ya kwamba Yesu ndiye Kristo: Mungu, Yule Mtiwa Mafuta.

Hakuna mtu anayejua mambo ya Mungu ila Roho wa Mungu na yeye ambaye Roho wa Mungu humfunulia hayo. Tunahitaji kumsihi Mungu kwa ajili ya ufunuo zaidi kuliko kitu kingine cho chote ulimwenguni. Tumeikubali Biblia, tumekubali zile kweli zake kuu, lakini ingali si halisi kwa watu walio wengi kwa sababu ufunuo wa Roho haupo. Neno halijahuishwa. Biblia inasema katika 2 Kor. 5:21 ya kwamba tumekuwa haki ya Mungu kwa muungano wetu na Yesu Kristo. Mlilipata? Inasema ya kwamba SISI NI HAKI YENYEWE YA MUNGU MWENYEWE kwa kuwa KATIKA KRISTO. Inasema ya kwamba Yeye (Yesu) alifanyika Dhambi kwa ajili yetu. Haisemi Yeye Mwenyewe akawa mwenye dhambi, lakini alifanyika DHAMBI kwa ajili yetu ili kwamba kwa kuungana kwetu na Yeye tuweze kufanyika HAKI ya Mungu. Kama tukikubali kweli hiyo (na hatuna budi kuikubali) kwamba Yeye alifanyika DHAMBI kweli kabisa kwa ajili yetu kwa kupachukua mahali petu, basi hatuna budi kukubali ukweli kwamba sisi kwa kuungana kwetu Naye tumekuwa HAKI YENYEWE ya Mungu. Kukataa hilo moja ni kukataa hilo lingine. Kukubali hilo moja ni kukubali hilo lingine. Sasa tunajua Biblia inasema hivyo. Haliwezi kukanushwa. Lakini ufunuo wake haupo. Si halisi kwa wengi wa watoto wa Mungu. Ni aya nzuri tu katika Biblia. Lakini tunahitaji ifanywe HAI kwetu. Hilo litahitaji ufunuo.

Hebu niweke hapa kitu ambacho kitashangaza na kukusaidia. Ni vigumu kumpata mwanafunzi ambaye haamini Agano Jipya kwanza kabisa lilikuwa katika lugha ya Kiyunani. Wanafunzi wetu wote maarufu wa Biblia wamesema ya kwamba Mungu aliupa ulimwengu mataifa makuu matatu waliotoa michango mikuu mitatu kwa ajili ya Injili. Alitupa Wayunani waliotupa lugha ya ulimwengu mzima. Alitupa Wayahudi waliotupa dini ya kweli na maarifa ya kweli kuhusu Mungu kwa njia ya Mwokozi. Alitupa Warumi waliotupa dola iliyo imara pamoja na sheria na utaratibu wa barabara kuu. Hivyo basi tuna dini ya kweli, lugha ya kuitangazia kwa watu wengi, na serikali na barabara za kuisambazia kwa njia za kawaida. Na tukinena kihistoria jambo hili linaonekana kuwa ni la kweli kabisa. Na siku hizi wasomi wetu wa Kiyunani wanasema ya kwamba lugha ya Kiyunani ya siku za Biblia ni kamilifu sana na sahihi sana hivi kwamba kama mwanafunzi wa Kiyunani ni mwanasarufi hodari sana na asiyekosea anaweza kujua kwa kweli sawasawa kabisa kile hasa Neno la Agano Jipya linachofundisha.

Je! Hii si ni nadharia tu? Je! Hii ni kweli? Je! sio kweli kwamba kila msomi wa lugha ya Kiyunani mwenye kutukuka kutoka kwenye madhehebu fulani hushindana na mwanafunzi mwingine wa madhehebu mengine, na je! sio kweli ya kwamba mabishano yao msingi wake ni juu ya maneno yale yale ya Kiyunani na kanuni zile zile za sarufi? Hakika hivyo ndivyo ilivyo. Hata huko nyuma katika Wakati wa Pergamo, kabla tu ya lile Baraza la Nikea la 325 kulikuwa na wanafunzi wawili mashuhuri sana, Ariusi na Athanasio waliokabana katika vita vya mafundisho juu ya neno moja la Kiyunani. Hoja yao ilikuwa kali sana na ikaenea ulimwenguni mwote hivi kwamba wanahistoria walisema ulimwengu ulikuwa umegawanyika katika vokali moja (sauti ya herufi mbili katika silabi moja.)

Sasa, kama Kiyunani ni kikamilifu namna hiyo, na kimechaguliwa kabisa na Mungu, mbona kumekuwa na ubishi kama huo? Hakika Mungu hakukusudia sisi sote kujua Kiyunani? Sasa hivi leo tuna mabishano juu ya Kiyunani. Chukua kwa mfano kile kitabu, "Kanisa la Kristo Lililolemaa Likipigwa Eksirei" kilichoandikwa na Dk. McCrossan. Ndani yake anaweka nukuu nyingi kutoka kwa wanasarufi wengi mashuhuri wa Kiyunani, na anathibitisha kuridhika kwake kwamba sheria zisizobadilika za sarufi ya Kiyunani zinathibitisha dhahiri kwamba Biblia inafundisha mtu kubatizwa kwa Roho Mtakatifu baada ya kuzaliwa upya. Pia yeye anasema yakini ya kwamba wanawake wanaweza kuchukua mimbara kwa sababu neno kutabiri linamaanisha kuhubiri. Lakini je! yeye amewashawishi wasomi wengine wa Kiyunani ambao ni hodari tu kama alivyo yeye? Kamwe. Yote unayopaswa kufanya ni kusoma wale wanafunzi ambao wana msimamo tofauti na kusikia nukuu zao walizojifunza.

Sasa si kwamba tu yale niliyosema ni ya kweli tu, bali hebu twende mbele zaidi. Leo tuna wanafunzi ambao wanadai ya kwamba yale maandiko ya kwanza yaliandikwa katika Kiaramu ambayo ilikuwa ndiyo lugha ya Yesu na ya watu wa siku Zake. Wao wanadai ya kwamba hao watu hawakuzungumza na kuandika katika Kiyunani kama inavyodhaniwa na watu wengi. Na ukweli ni kwamba wanahistoria wetu wamegawanyika juu ya jambo hilo. Kwa mfano, Dk. Schonfield, msomi hodari sana amejiridhisha kwa kuthibitisha kutokana na utafiti kwamba Agano Jipya liliandikwa katika lugha ya kienyeji ya watu wanaozungumza Kiyunani wa siku hizo. Yeye anajenga hoja safi kwa imani zake, kutokana na hati mbalimbali alizopata. Lakini kwa upande mwingine tuna mwanafunzi mwingine mashuhuri, Dk. Lamsa, ambaye ameshawishika ya kwamba Agano Jipya liliandikwa katika Kiaramu na hana mwingine ila mwanahistoria maarufu sana, Toynbee, kuunga mkono mjadala wake kwamba Kiaramu, wala SI KIYUNANI ndiyo iliyokuwa lugha ya watu hao, kwa hiyo inaonekana ya kwamba inawezekana Agano Jipya liliandikwa

kwanza katika Kiaramu.

Hata hivyo, kabla hatujashughulikia jambo hili sana, hebu na tusome tafsiri ya King James na tafsiri ya Dk. Lamsa pia. Tunafurahi kuona ya kwamba maneno katika hizo zote mbili ni yale yale kabisa hivi kwamba kwa kweli hakuna tofauti kati ya yaliyomo wala katika mafundisho. Hata tunaweza kuitimisha kwamba Mungu ameruhusu maandiko haya yaliyovumbuliwa hivi karibuni na vitabu vilivyoandikwa hivi karibuni vya maandiko ambayo tayari yamejulikana kuja mbele zetu kuthibitisha ukweli wa kile tulicho nacho tayari. Nasi tunaona ya kwamba ingawa watafsiri wanaweza kupingana, maandiko hayapingani.

Sasa unaweza kuona ya kwamba huwezi kuweka msingi wa tafsiri juu ya maarifa ya kina sana ya msomi juu ya lugha ambayo Biblia imeandikwa. Lakini kama wewe bado huwezi kuona hilo kwa sababu umetiwa utaji katika moyo wako na mapokeo hapa pana mfano mmoja wa mwisho. Hakuna mtu anayeweza kutilia shaka kwamba Waandishi na Mafarisayo na wanachuoni mashuhuri wa mwaka wa 33 B.K. walijua kanuni sahihi za sarufi na maana sahihi ya maneno ambayo kwayo Agano la Kale liliandikwa; lakini pamoja na maarifa yao ya hali ya juu sana walikosa ufunuo wa Neno la Mungu lililoahidiwa lililodhihirishwa katika Mwana. Alikuwa yuko hapo na ameelezewa kutoka Mwanzo hadi Malaki, kukiweko na sura zote nzima zilizotengwa kwa ajili Yake na huduma Yake, na hata hivyo kuacha wachache walioangaziwa na Roho, walimkosa kabisa.

Sasa tunafikia neno la uamuzi wa mwisho, uamuzi wa mwisho ule ambao tuliupata tayari katika Neno. Hata ingawa tunaamini katika kujaribu kupata maandiko ya kale sana na yaliyo bora sana ili kupata kumbukumbu nzuri sana iwezekanayo ya Neno, hatutaweza kupata maana yake halisi kwa kusoma na kulinganisha Maandiko, hata tuwe waaminifu tuwezavyo kuwa. ITAHITAJI UFUNUO KUTOKA KWA MUNGU KULIELEZA. HIVYO NDIVYO HASA PAULO ALIVYOSEMA, "NAYO TWAYANENA; SI KWA MANENO YANAYOFUNDISHWA KWA HEKIMA YA KIBINADAMU, BALI YANAYOFUNDISHWA NA ROHO MTAKATIFU." I Kor. 2:15. Ufunuo wa kweli ni Mungu akifasiri Neno Lake Mwenyewe kwa kuthibitisha yale yaliyoahidiwa.

Sasa mtu asielewe vibaya na yale niliyosema na kufikiria ya kwamba mimi siamini katika usahihi wa Neno jinsi tulivyo nalo sasa. Ninaamini Biblia hii ni sahihi. Yesu alishuhudia kabisa ukweli wa Agano la Kale alipokuwa hapa duniani nalo liliandikwa vile vile kama Agano letu Jipya. Usije ukakosea, tuna Neno lisilokosea la Mungu leo na mtu ye yote asithubutu kuondoa kwake ama kuongeza kwake. Lakini tunahitaji Roho yule yule aliyetupa hilo, kutufundisha.

Loo, jinsi tunavyohitaji ufunuo kwa Roho. Hatuhitaji Biblia mpya, hatuhitaji tafsiri mpya, ingawa baadhi ni nzuri sana, wala sizipingi, LAKINI TUNAHITAJI UFUNUO WA ROHO. Na Mungu ashukuriwe, tunaweza kupata kile tunachohitaji, kwa kuwa Mungu anataka kutufunulia Neno Lake kwa Roho Wake.

Mungu na aanze kwa Roho Wake kutupa ufunuo unaotoa uzima na wenye ushindi daima. Loo! laiti kanisa lingalipata tu ufunuo mpya na liwe kwa ufunuo huo Neno linaloishi lililodhihirishwa, tungeweza kufanya kazi kuu zaidi na kumtukuza Mungu Baba yetu wa mbinguni.

**Kufunguliwa Kutoka Dhambini**

Ufunuo 1:5,

"Yeye atupendaye, na kutuosha dhambi zetu katika damu Yake."

Neno "kutuosha" kwa kweli ni "kutufungua"_"Kutufungua kutoka katika dhambi zetu kwa damu Yake Mwenyewe." Hiyo si ni ya ajabu? Lakini je! wewe una ni wa kiroho? Ulilipata? Damu Yake MWENYEWE ndiyo iliyotufungua kabisa kutoka katika dhambi zetu. Haikuwa damu ya mwanadamu. Ilikuwa ni damu ya Mungu. Petro aliiita damu ya Kristo. Paulo aliiita damu ya Bwana, na damu ya Yesu. Si watu watatu, bali mtu MMOJA. Huo hapo huo ufunuo tena, MUNGU MMOJA. Huyo Yehova Mungu mwenye nguvu zote alishuka na kujifanyia Mwenyewe mwili kwa njia ya kuzaliwa kibikira na kukaa ndani ya mwili huo, ili iwe ni damu ya Mungu ambayo ingetufungua (kutufungua kabisa) kutoka katika dhambi zetu na kutuweka mbele Yake Mwenyewe bila waa kwa furaha kuu.

Ungetaka mfano wa Agano la Kale? Hebu na turudi kwenye Bustani ya Edeni. Wakati habari ya kwanza ilipotukuka ya kwamba mwana, Adamu, alikuwa amepotea, je! Mungu alimtuma malaika? Je! Yeye alimtuma mwana? Je! Yeye alimtuma mwingine kama sisi? La, Yeye alikuja Mwenyewe kumkomboa huyo mwana aliyepotea. Haleluya! Mungu hakuweka mpango Wake wa wokovu kwa mwingine. Alijiamini Mwenyewe tu. Mungu alifanyika mwili akakaa kwetu na kutukomboa kwa ajili Yake Mwenyewe. Tunaokolewa kwa "damu ya Mungu". Mungu wa Milele aliishi ndani ya mwili unaopatikana na mauti ili kuondoa dhambi. Yeye alifanyika Mwana-Kondoo kusudi amwage damu Yake na kuingia katika pazia pamoja nayo.

Fikiria hili. Kwa kuwa ni damu ya Mungu, ni damu iliyo kamilifu; na kama damu iliyo kamilifu inatufungua kutoka kwenye nguvu na kifungo na kuchafuliwa na dhambi, basi kule kufunguliwa ni kukamilifu na kamili. Kwa hiyo sasa hakuna hukumu ya adhabu.

"Ni nani atakayewashtaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye anayehesabia haki (anayetutangaza kuwa wenye haki). Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo ndiye aliyekufa …"

Warumi 8:33-34.

Hilo hapo, mauti Yake ilitupa damu. Damu imetufungua. Sasa hakuna hukumu ya adhabu. Inawezekanaje kuweko? Hakuna kitu cha kuhukumiwa, kwa sababu damu imetufungua kutoka dhambini. Sisi ni huru, hatuna hatia. Usimsikilize mwanadamu, sikiliza Neno. Umefunguliwa kwa damu.

Sasa msifungwe tena na mapokeo na kanuni za imani na madhehebu. Usidanganywe kwa kuwasikiliza wale wanaokana nguvu za Neno na kukana ya kwamba Yesu huokoa, huponya, hujaza Roho Mtakatifu na nguvu. Ninyi ni watu huru wa Mungu, mliofunguliwa kwa damu Yake Mwenyewe. Kama ungali unashikilia imani yako kwenye kanuni za imani na madhehebu, ni dhahiri kwa huo ushuhuda ya kwamba umepoteza imani yako katika Neno.

**Wafalme Na Makuhani**

Ufunuo 1:6,

"Na kutufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu, na Baba Yake; Utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele. Amina."

"Yeye ametuumba!" Loo, kuna kweli fulani tunazopaswa kusisitiza. Hii ni mojawapo. YEYE! AMETUFANYA! Wokovu ni kazi Yake. Wokovu ni wa Bwana. Wote ni wa neema yote. Yeye alitukomboa kwa kusudi fulani. Yeye alitununua kwa kusudi fulani. Sisi ni wafalme, wafalme wa kiroho. Loo, tutakuwa wafalme juu ya nchi pamoja Naye wakati atakapoketi kwenye kiti Chake cha enzi. Lakini sasa sisi ni wafalme wa kiroho na tunatawala juu ya ufalme wa kiroho.

Inasema katika Warumi 5:17,

"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja; zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo."

Na katika Wakolosai 1:13,

"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme (utawala) wa Mwana wa pendo Lake."

Sasa hivi tunatawala pamoja na Kristo, tukitawala dhambi, ulimwengu, mwili, na Ibilisi. Akionyesha sifa Zake na utukufu; akijionyesha Mwenyewe, kwa kuwa ni Kristo ndani yetu, akipenda na kufanya mapenzi Yake mema. Naam, hakika, hata sasa tumeketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu.

"Na kutufanya makuhani." Naam, makuhani Kwake, wakitoa sifa za kiroho za midomo iliyotakaswa. Tunayatumia maisha yetu kama sadaka tamu Kwake. Kumwabudu katika Roho na kweli. Tukipatanisha na kuombeana dua. Makuhani na wafalme kwa Mungu wetu. Si ajabu ulimwengu hautuvutii nasi ni watu wa ajabu wenye bidii mno katika kutenda mema. Tumeumbwa upya katika Yeye tupate kuwa watoto tufananao na Baba yetu.

**Mungu Ajaye**

Ufunuo 1:7,

"Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao pia waliomchoma: na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili Yake. Naam. Amina."

Yeye yuaja. Yesu anakuja. Mungu anakuja. Nabii anakuja. Kuhani na Mfalme anakuja. Aliye YOTE katika YOTE anakuja. Naam, Bwana Yesu, njoo upesi. Amina.

Yeye yuaja. Yeye anakuja katika mawingu, mawingu ya utukufu kama wakati alipoonekana juu ya Mlima wa Kugeuzwa, na mavazi Yake yalikuwa yaking'aa wakati nguvu za Mungu zilipomfunika. Na KILA jicho litamwona. Hiyo inamaanisha hii si kule Kunyakuliwa. Huu ndio wakati atakapokuja kuchukua mahali pake panapofaa kama Mtawala wa Ulimwengu. Huu ni wakati ambapo hao waliomchoma kwa kanuni zao za imani na mafundisho ya madhehebu yao watakapoomboleza, na watu wote watalia kwa hofu kwa sababu ya Yeye Ambaye ni Neno.

Hii ndiyo hadithi ya ufunuo ya Zekaria 12:9-14. Zekaria alitabiri jambo hili yapata miaka 2500 iliyopita. Liko karibu kutukia. Sikilizeni.

"Hata itakuwa siku hiyo, ya kwamba nitatafuta kuwaangamiza mataifa yote watakaokuja kupigana na Yerusalemu.

Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, Roho ya neema na kuomba: nao watanitazama Mimi Ambaye walinichoma ..."

Sasa, Injili itawarudia lini Wayahudi? Wakati siku ya Mataifa itakapokwisha. Injili iko tayari kurudi kwa Wayahudi. Loo, laiti ningaliweza tu kuwaambia jambo fulani ambalo liko karibu kutukia katika siku yetu hii. Jambo hili kuu lililo karibu kutukia litaendelea mpaka Ufunuo 11 na kuwachukua wale mashahidi wawili, wale manabii wawili, Musa na Eliya, wakiirudisha Injili kwa Wayahudi. Tuko tayari kwa ajili ya jambo hilo. Kila kitu kiko katika utaratibu. Kama vile Wayahudi walivyouleta ujumbe kwa Mataifa, vivyo hivyo Mataifa wataurudisha moja kwa moja kwa Wayahudi, ndipo Kunyakuliwa kutakuja.

Sasa, kumbukeni yale tuliyoyasoma katika Ufunuo na Zekaria. Yote yanatukia mara baada ya ile dhiki. Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza halipiti kwenye ile dhiki. Tunajua jambo hilo. Biblia inafundisha jambo hilo.

Wakati huo inasema ya kwamba Mungu atamwaga Roho Wake juu ya nyumba ya Israeli. Ni Roho yule yule aliyemwagwa juu ya Mataifa katika siku zao. "Nao watanitazama Mimi Ambaye walimchoma, nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee, nao wataona uchungu kwa ajili Yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza. Siku hiyo kutakuwa na maombolezo makuu huko Yerusalemu, kama maombolezo ya Hadadrimoni katika bonde la Megido. Nayo nchi itaomboleza, kila jamaa peke yake; jamaa ya nyumba ya Daudi peke yao, na wake zao peke yao; jamaa ya nyumba ya Nathani peke yao, na wake zao peke yao^" na kila moja ya hizo nyumba peke yao wakati Yeye atakapokuja katika mawingu ya utukufu katika Kuja Kwake Mara ya Pili. Wale Wayahudi waliomchoma watamwona kama isemwavyo katika Maandiko mengine, "Ulipata wapi jeraha hizo?" Naye atasema, "Katika nyumba ya rafiki Zangu." Hautakuwa tu ni wakati wa maombolezo kwa Wayahudi waliomkataa kama Masihi, bali utakuwa ni wakati wa maombolezo kwa wale waliosalia wa Mataifa ambao wamemkataa kama Mwokozi wa siku hii.

Kutakuwako na kulia na kuomboleza. Wanawali waliolala watakuwa wakiomboleza. Wao wanawakilisha kanisa lililokataa kupata mafuta (ishara ya Roho Mtakatifu) katika taa zao (alama ya mwili ama chombo cha mafuta) mpaka ikawa wamechelewa. Si kwamba wao hawakuwa ni watu wazuri. Wao walikuwa wanawali na hilo linaonyesha hali ya juu ya uadilifu. Lakini wao hawakuwa na mafuta katika taa zao kwa hiyo wakatupwa nje ambako kulikuwa na kulia na kusaga meno.

Hebu tufananishe haya yote kutoka katika Mwanzo, sura ya 45, ambapo Yusufu anakutana na ndugu zake huko Misri na anajifunua kwao. Mwanzo 45:1-7, "Hapo Yusufu hakuweza kujizuia mbele yao wote waliosimama karibu naye; akapiga kelele, na kusema, Mwondoeni kila mtu mbele yangu. Wala hakusimama mtu pamoja naye, Yusufu alipojitambulisha kwa nduguze. Akapaza sauti yake akalia: nao Wamisri na watu wa nyumba ya Farao nao wakasikia. Yusufu akawaambia ndugu zake, Mimi ndimi Yusufu; baba yangu angali hai? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu; maana waliingiwa na hofu mbele yake. Yusufu akawaambia ndugu zake, Njooni karibu nami, nawaomba. Nao wakakaribia. Akasema, Mimi ni Yusufu, ndugu yenu, ambaye mliniuza kwenda Misri. Basi sasa msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku: maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu. Maana miaka hii miwili njaa imekuwa katika nchi: na iko tena miaka mitano, isiyo na kulima wala kuvuna. Mungu alinipeleka mbele yenu kuwahifadhia masazo katika nchi, na kuwaokoa ninyi kwa wokovu mkuu."

Sasa hilo halilingani na Zekaria 12 kwa uzuri tu? Tukiweka hayo mawili pamoja hatuna budi kuyaweka sawa kabisa.

Wakati Yusufu alipokuwa mdogo sana alichukiwa na ndugu zake. Kwa nini alichukiwa na ndugu zake? Ilikuwa ni kwa sababu alikuwa wa Kiroho. Hakuweza kujizuia kuona maono hayo, wala hakuweza kusaidia kuota ndoto na kufasiri. Hilo lilikuwa ndani yake. Asingeweza kuonyesha kitu kingine cho chote ila kile kilichokuwa ndani yake. Kwa hiyo, wakati nduguze walipomchukia ilikuwa hakuna sababu. Lakini yeye alikuwa mpendwa wa baba yake. Baba yake alikuwa nabii na alielewa. Hilo linafanya mfano mkamilifu wa Kristo. Mungu Baba alimpenda Mwana, lakini wale ndugu (Waandishi na Mafarisayo) walimchukia kwa sababu Yeye aliweza kuwaponya wagonjwa, kufanya miujiza na kutabiri mambo yajayo, kuona maono na kuyafasiri. Hiyo haikuwa sababu ya kumchukia bali wao walimchukia, na kama vile ndugu za Yusufu, wao walimchukia bila sababu.

Sasa kumbuka jinsi hao wana wa Yakobo walivyomtendea Yusufu. Walimtupa shimoni. Wakachukua koti lake la rangi nyingi ambalo baba yake alikuwa amempa na kulichovya katika damu kumfanya baba yake afikirie kwamba huyo mvulana aliuawa na mnyama fulani. Walimuuza kwa wafanyi biashara ya watumwa ambao walimchukua mpaka Misri na huko akauzwa tena kwa jemadari. Mke wa huyo jemadari alimfanya afungwe gerezani kwa kumsingizia, lakini baada ya kitambo kidogo uwezo wake kama nabii ulimfanya Farao asikie habari zake naye akainuliwa hadi mkono wa kuume wa Farao akiwa na mamlaka makubwa hivi kwamba hakuna mtu angaliweza kumkaribia Farao isipokuwa aje kwanza kwa kupitia kwa Yusufu.

Sasa hebu na tuyachunguze maisha ya Yusufu alipokuwa Misri, kwa maana hapa ndipo tunamwona

kama mfano mkamilifu wa Kristo. Akiwa katika nyumba ya jemadari alishtakiwa kwa uongo, akaadhibiwa na kufungwa gerezani bila sababu, kama tu walivyomfanyia Yesu. Huko gerezani alifasiri ndoto ya mkuu wa wanyweshaji na ya mwokaji waliokuwa pia wafungwa pamoja naye. Mnyweshaji aliachiliwa hai, bali huyo mwingine alihukumiwa adhabu ya kifo. Kristo alifungwa msalabani, akaachwa na Mungu na wanadamu. Pande zote mbili Zake kulikuwa na mwizi—mmoja alikufa, kiroho, bali huyo mwingine alipewa uzima. Basi angalia, wakati Yesu alipotolewa msalabani, Yeye aliinuliwa hadi mbinguni na sasa anaketi mkono wa kuume wa ile Roho kuu ya Yehova; wala hakuna mtu awezaye kuja kwa Mungu ila kwa Yeye. Kuna mpatanishi Mmoja kati ya Mungu na wanadamu, na Yeye ndiye tu unayehitaji. Hakuna akina Mariamu wala watakatifu, ni Yesu tu.

Tukiendelea na mfano huu tunaouona katika Yusufu, angalia jinsi ambavyo kila kitu alichokifanya huko Misri kilifanikiwa. Kazi yake ya kwanza kwa yule jemadari ilifanikiwa. Hata gereza lilifanikiwa. Wakati Yesu atakaporudi, jangwa litachanua kama waridi. Yeye ni "Mwana wa Usitawi." Kwa kuwa hakuna wakati uliopata kusitawi kama ule uliokuwa chini ya Yusufu, vivyo hivyo kuna wakati wa baraka kama hizo unaokuja duniani ambao ulimwengu haujapata kuujua. Kila mmoja wetu anaweza kuketi chini ya mtini wake mwenyewe na kucheka na kufurahi na kuishi milele katika uwepo Wake. Katika uwepo Wake kuna utimilifu wa furaha na katika mkono Wake wa kuume kuna raha za milele na milele. Mungu asifiwe.

Sasa angalia, kwamba kila mahali Yusufu alipoenda walipiga tarumbeta kutangaza kuwasili kwake. Watu wangepiga kelele, "Mpigieni goti Yusufu!" Haidhuru mtu alikuwa akifanya nini, wakati hiyo baragumu ilipolia alipiga magoti. Angeweza kuwa anauza bidhaa fulani mitaani, akikaribia kuchukua pesa zake, lakini ilimbidi kuacha na kupiga goti wakati baragumu hiyo ilipolia. Kama yeye alikuwa mchezaji ama mwigizaji wa mchezo, ingembidi kukomesha mchezo wake na kumpigia Yusufu magoti wakati uwepo wake ulipotangazwa kwa wito wa hiyo baragumu. Na moja ya siku hizi kila kitu katika wakati kitasimama kimya hapo baragumu ya Mungu itakapolia, na waliokufa katika Kristo watafufuka na itapambazuka asubuhi ya milele inayong'aa na iliyo nzuri. Kila kitu kitapiga magoti wakati huo, kwa maana imeandikwa,

"Kwa hiyo Mungu pia amemtukuza sana, na kumpa Jina lipitalo kila jina;

ili kwa Jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi;

Na kila ulimi ukiri ya kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Wafilipi 2:9-11.

Lakini angalia ufunuo mwingine mtukufu katika mfano huu wa Yusufu. Yusufu, alipokuwa Misri, alipewa bibiarusi wa Mataifa na kwake akapata jamaa ya wana wawili, Efraimu na Manase. Yusufu alimwomba baba yake awabariki hao wavulana wawili. Akawaweka mbele ya Yakobo ili kwamba Manase, mzaliwa wa kwanza angekuwa kwenye mkono wa kuume wa Yakobo na Efraimu mkono wa kushoto. Yakobo alipokuwa tayari kuwabariki akapitanisha mikono yake hivi kwamba mkono wa kuume ulimwangukia aliye mdogo. Yusufu alipaza sauti, "Sivyo, baba, huyu ni mzaliwa wa kwanza mkono wako wa kulia." Lakini Yakobo akasema, "Mungu aliipishanisha mikono yangu." Hapa katika mfano tunaona ya kwamba baraka ambazo zilikuwa ni za mzaliwa wa kwanza (Myahudi) zilipewa aliye mdogo (Mmataifa) kupitia msalaba (mikono iliyopishanishwa) wa Bwana Yesu Kristo. Baraka huja kupitia msalabani. Gal.3:13-14, "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu: maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti; ili kwamba baraka ya Ibrahimu iwafikilie Mataifa katika Yesu Kristo; tupate kupokea ahadi ya Roho kwa njia ya imani." Baraka ya Ibrahimu ilikuja kwa njia ya msalaba kwa Mataifa. Wayahudi waliukataa msalaba; kwa hiyo, Yesu alimchukua Bibi-arusi Mmataifa.

Sasa tukirudi kwenye hadithi ya Yusufu kukutana na ndugu zake. Mnakumbuka ya kwamba si ndugu wote waliokuja. Yusufu alijua jambo hilo na akasisitiza ya kwamba ndugu wote wasimame mbele zake, la sivyo hangeweza kujitambulisha kwao. Hatimaye wakamleta yule aliyekuwa amekosekana, Benyamini mdogo. Ilikuwa ni Benyamini mdogo, ndugu wa tumbo moja wa Yusufu, aliyeiwasha moto nafsi yake. Na hapo Yusufu wetu, ambaye ni Yesu, atakapowajia watu ambao wameshika amri za Mungu na ambao wamerudi Palestina, nafsi Yake itawaka moto. Mtoto Benyamini anawakilisha Waisraeli 144,000 kutoka kila mahali duniani waliorudi Palestina kwa ajili ya ukombozi wao. Wao watakuwa wamesimama kule wakiwa tayari kumpokea Yeye, Ambaye kumjua vizuri ni Uzima wa milele. Watasema, "Huyu ndiye Mungu wetu Ambaye tumemngojea." Ndipo watamwona Yeye ambaye wamemchoma. Nao watalia kwa hofu, "Haya makovu mabaya sana yalitoka wapi? Ilitukiaje?" Nao watalia na kuomboleza, kila jamaa peke yao, kila mmoja peke yake katika uchungu wa huzuni.

Sasa Kanisa la Mataifa litakuwa wapi wakati Yesu anajitambulisha kwa ndugu Zake? Kumbukeni ya kwamba bibi-arusi wa Yusufu pamoja na wale watoto wawili walikuwa katika jumba la kifalme, kwa kuwa Yusufu alikuwa ameamuru, "Kila mtu na aniache; waondoe wote mbele zangu." Kwa hiyo bibi-arusi Mmataifa alikuwa amefichwa katika jumba la kifalme la Yusufu. Kanisa la Mataifa litaenda wapi katika kunyakuliwa? Katika jumba la kifalme. Bibi-arusi ataondolewa duniani. Atanyakuliwa kabla ya ile dhiki kuu kumlaki Bwana wake hewani. Kwa miaka mitatu na nusu wakati hasira ya kupatiliza ya Mungu inamiminwa, atakuwa katika ile Karamu Kuu ya Arusi ya Mwana-Kondoo. Ndipo Yeye atarudi, akimwacha

bibi-arusi Wake katika “nyumba ya Baba Yake,” wakati akijitambulisha kwa ndugu Zake. Katika wakati huu huu, agano la mpinga-Kristo ambalo Wayahudi wamefanya na Rumi litavunjwa. Rumi na marafiki zake basi wanatuma majeshi yao kuwaangamiza Wayahudi wote wanaomcha Mungu, na kulitii Neno.

Lakini wakati wanapokuja kuuvamia ule mji wapate kuuangamiza, kutatokea mbinguni ishara ya kuja Kwake Mwana wa Adamu akiwa na majeshi Yake yenye nguvu nyingi kuwaangamiza hao ambao wamekuwa wakiiharibu dunia. Huku adui amefukuzwa, Yesu basi anakuja na kujionyesha kwa wale 144,000. Baada ya kuona matendo Yake makuu ya wokovu, wamekuja kujua uweza Wake. Lakini pia kwa kuyaona majeraha Yake na wakijua ya kwamba walikuwa wamemkataa hata mpaka wakati huo, kunawafanya walie sana katika uchungu wa hofu kuu na woga, kama walivyofanya ndugu zao wa kale waliposimama mbele ya Yusufu, wakiogopa sana kwamba wangeuawa. Lakini kama vile Yusufu alivyosema, “Msijikasirikie. Ni sawa. Mungu alikuwa katika hayo yote. Alifanya hivyo kuhifadhi uhai.” Vivyo hivyo Yesu atanena amani na upendo kwao.

Kwa nini Wayahudi walimkataa Yesu? Mungu alikuwa katika hayo yote. Ilikuwa ndiyo njia pekee angaliweza kumleta bibi-arusi wa Mataifa. Alikufa msalabani kuhifadhi maisha ya Kanisa la Mataifa.

Sasa hawa 144,000 hawako katika bibi-arusi. Katika Ufunuo 14:4 wanaitwa wanawali nao wanamfuata Mwana-Kondoo kokote aendako. Ukweli kwamba wao hawajatiwa unajisi na wanawake inaonyesha ya kwamba wao ni matowashi (Mat. 19:12). Matowashi walikuwa wasimamizi wa vyumba vya bibiarusi. Walikuwa ni wahudumu. Angalia kwamba hawaketi kwenye kiti cha enzi bali wako mbele ya kiti cha enzi. La, wao hawako katika bibi-arusi, bali watakuwa katika ule utawala wa fahari wa miaka elfu moja.

Tunaona basi ya kwamba wakati hawa wa mwisho wa Israeli watakapounganishwa kwa Bwana katika upendo, na yule adui amekwisha kuangamizwa, Mungu atautayarisha ule mlima Wake mtakatifu, ile Bustani Yake mpya ya Edeni kwa ajili ya bibi-arusi Wake na watumishi Wake kwa ajili ya fungate ya miaka elfu moja duniani. Kwa kuwa Adamu na Hawa walikuwa katika ile bustani na hawakuimaliza ile miaka elfu moja, sasa Yesu, Adamu wetu wa mwisho, na Hawa Wake (Kanisa la Kweli) atatimiza mpango wote wa Mungu.

Loo, jinsi Biblia inavyojirudia. Tukio la Yusufu na ndugu zake liko karibu na kurudiwa, kwa maana Yesu yuaja hivi karibuni.

Na tunapoacha mfano wa Yusufu, kuna jambo moja zaidi ninalotaka kulileta mlione kuhusu wakati huu wa mwisho. Mnakumbuka ya kwamba wakati Yusufu aliposimama mbele ya ndugu zake wakati Benyamini alipokuwa hayuko pamoja nao alizungumza kupitia mkalimani ingawa yeye alijua Kiebrania vizuri. Alizungumza na ndugu zake katika lugha ya kigeni. Hivi mlijua ya kwamba ule Wakati wa kwanza wa Mataifa (kichwa cha dhahabu, Kipindi cha enzi ya Babeli) ulimalizika kwa ukiwa na ujumbe katika lugha zilioandikwa kwenye ukuta? Wakati huu unaisha namna ile ile. Wingi wa lugha katika siku hii ni thibitisho zaidi ya kwamba Majira ya Mataifa yamekwisha na Mungu anawarudia Israeli.

Yeye yuaja upesi. Alfa na Omega, Nabii, Kuhani na Mfalme, Yote katika Yote, Bwana Mungu wa Majeshi, yuaja upesi. Naam Bwana Yesu, Mungu Mmoja na Aliye wa Kweli, njoo upesi!

MESSAGE hub online

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7

www.messagehub.info